


Share a story today!

Nalibali
INAANZA KWA
HADITHI.

Siku ya Kusoma kwa Sauti Duniani Inayoandaliwa wa Nal'ibali



Mwaka huu unawakilisha **maadhimisho ya 10 ya kila mwaka** ya kampeni ya Nal'ibali ya Siku ya Kusoma kwa Sauti Duniani! Tunakualika wewe pamoja na familia yako msome hadithi yetu maalum ya, *Tafrija kwenye bustani*, kwa sauti. Imeandikwa na Mabel Mnensa na michoro imechorwa na Rico.

Hadithi hii inapatikana kwa lugha zote 11 rasmi za Afrika Kusini. Na, ili kuruhusu watu wengi kadri iwezekanavyo kufurahia hadithi yetu ya Siku ya Kusoma kwa sauti Duniani kwa lugha yao ya nyumbani, hadithi hii pia inapatikana kwa lugha ya **Kishona, Kifaransa, Kichewa, Kireno, Kiswahili** na **Kilingala**.

Tusaidie kusoma hadithi kwa sauti kwa watoto wengi kadri iwezekanavyo Siku hii ya Kusoma kwa Sauti Duniani, tarehe **2 Februari 2022** – na kila siku – na uwe sehemu ya mpango wa kukuza kiwango cha kujua kusoma na kuandika nchini Afrika Kusini!



Kuza moyo wa kupenda kusoma pamoja

Unapofurahia hadithi na watoto wako kila siku, hali hiyo:

- ★ inawaonyesha kwamba unachukulia suala la vitabu na kusoma kuwa muhimu.
- ★ inakupa mambo ya kuzungumzia kama familia.
- ★ inakuza uhusiano thabiti kati yenu.
- ★ inawasaidia kuona kwamba kusoma ni shughuli ya kufurahisha na yenye manufaa.
- ★ inawaonyesha jinsi tunavyosoma na jinsi vitabu hutumika.
- ★ inawaruhusu wafurahie hadithi ambazo bado hawawezi kujisomea wenyewe.
- ★ inawatia moyo wa kujifunza kujisomea kisha kuendelea kusoma.
- ★ inasadia kukuza kiwango cha kujua kusoma na kuandika na maarifa ya kihisia ili waweze kukabiliana vyema na hali za shuleni na katika jamii.

Cha kufanya

Ahidi kwamba mtasoma pamoja kwa sauti kama familia **Siku hii ya Kusoma kwa Sauti Duniani** – na kila siku. Jisajili katika tovuti ya www.nalibali.org au tuma neno “WRAD” kupitia WhatsApp kwa nambari **060 044 2254**. Kila familia itakayoajisajili itapata fursa ya kujiunga na mchakato wa kusoma kama **familia wa kampeni ya Nal'ibali ya Siku ya Kusoma Kwa Sauti Duniani**. Utapokea hadithi za ziada pamoja na vidokezo na mawazo kuhusu jinsi ya kusoma na watoto wako mwaka mzima.



**Eneza upendo wa hadithi!
Sambaza hii hadithi au uishiriki
na mtu unayemfahamu.**



Tafrija kwenye bustani

Hadithi kutoka Mabel Mnensa ★ Michoro kutoka Rico ★ Imetafsiriwa na Afrolingo

Neo, Josh na Hope walikuwa wote kwa nyumba ya Gogo. Walikuwa wanaongea na kucheka kwa sauti.



"Shhhh!" Gogo alisema. "Siwezi kusikia kile wanachosema kwenye redio. Kujeni, hebu sisi sote tusikize kipindi ninachokipenda zaidi."

Kila mtu alinyamaza na kusikiliza. Kwa ghafla, walisikia mtangazaji akitaja jina la bustani yao.

"Ala! Bustani yetu inajulikana sana!" Neo alisema.

"... na Tiniso, anayejulikana pia kama Tin, atakuwa na maonyesho kwenye bustani hiyo jioni hii akiwa na bendi la We Can Band. Wasanii kutoka Zimbabwe, Nigeria na Malawi wataburudisha kwenye jukwaa. Kila mtu anakaribishwa kwenye tafrija hiyo!" mtangazaji alisema.

"Gogo," Neo alisema, "umesikia matangazo hayo? Wamesema kila mtu anakaribishwa.

Tafadhali tuhudurie tafrija hiyo? Tafadhali?"

Gogo alimwalia Neo na kutabasamu. "Ikiwa Josh na Hope wataruhusiwa kuhudhuria, basi mnaweza kuhudhuria pia," alisema. Josh na Hope waliondoka upesi kuenda kuomba wazazi wao ruhusa wahudhurie tafrija kwenye bustani.

Waliporudi kumchukua Neo, Hope alimwambia Gogo kuwa Bella na mamake wangehudhuria tafrija hiyo pia.

"Sawa, mhudhurie basi. Mkae pamoja mkiwa huko," Gogo alisema.

Kwenye bustani, Neo alimuona Bella na mamake, na hata Noodle alikuwa amekuja na wao. "Nafikiri kila mtu kutoka eneo letu yuko hapa," Neo alisema. "Na baadhi ya wageni pia."

"Sikiliza..." Josh alisema. "Kuna watu wanaozungumza Kifaransa?"

"Ndiyo!" Hope alisema. "Naweza kusikia lugha ya Chichewa na Shona pia."

Neo alishika mkono wa Hope. "Tazama," Neo alisema, "Msanii Tin anaburudisha jukwaani! Lakini wapi bendi la We Can Band?"

Hata kabla Hope aweze kujibu, Tin alikaribia kwenye mikrofoni. "Hamjambo!" Tin alisema. "JE, MKO TAYARI KUWANZA TAFRIJA HII?"

"Yebo, ndiyo!" umati ulijibu kwa sauti.

Tin alianza kucheza gitaa yake. "Rudia ninayosema," alisema huku akianza kuimba. "Mguu wa kushoto nyuma."




"Mguu wa kushoto nyuma," umati uliimba.

"Mguu wa kushoto kulia," Tin aliimba.

"Mguu wa kushoto kulia," umati uliimba.

Josh na Hope walikuwa wanatabasamu na kuimba, lakini Neo alikuwa anatafuta bendi lile.



"Changamkeni!" Tin alisema kwa sauti. "Hebu tusherehekee! Ama mnahitaji bendi la We Can Band iwasaidie?"

"Yebo, ndiyo!" umati ulijibu kwa sauti.

Tin aliangalia hapa na pale. "Bendi la We Can Band liko wapi? Ah hapana, siioni bendi hilo hapa. Tafrija haitafurahisha bila bendi. Nitahitaji usaidizi. Timu pekee ndiyo inayoweza kutimiza ndoto hii!" Tin alitabasamu huku akiangalia umati. "Kwanza, nitahitaji wapiga-ngoma wawili."

Neo na Hope walikuwa wa kwanza kuweka mikono yao juu. Walipopanda kwenye jukwaa, Tin aliwapeleka kwa mikebe minne ya kahawa iliyo na vifuniko vya plastiki. Mikebe hiyo yalipambwa kwa karatasi inayong'aa na vitufe. Pia kulikuwa na mikwirowa kutumiwa na Neo na Hope.

"Sasa tunahitaji mtikisaji," Tin alisema.

"Josh! Mwrite Josh!" Neo alisema kwa sauti.

"Kuna Josh kwenye umati huu? Josh yuko wapi? Hebu tumsaidie apande hapa jukwaani," Tin alicheka.

Josh aliweka mkono wake juu. Wanaume wawili waliinua kiti chake cha magurudumu hadi jukwaani.

"Karibu, Josh," Tin alisema. "Jaribu hawa watikisaji wawili."

Josh alitikisa kifaa kimoja na kisha kutikisa kingine. Vifa hivyo vilitoa sauti tofauti.

"Hiyo ni vyema," Tin alisema. "SASA, TAFRIJA..."

Lakini kabla aseme hayo, kulikuwa na sauti kubwa ya kengele. Kila mtu aliangalia hapa na pale kuona kilikuwa ni nini.

Kisha Noodle alikimbia jukwaani, akivuta mikebe iliyofungwa pamoja na uzi.

"Sauti za seti ya kengele!" Tin alisema kwa sauti. "Nilidhani nimepoteza."

Bella alikimbia kuelekea jukwaani. "Noodle!"

aliita. Noodle alikimbia kwenye Bella yuko, mikebe ikitoa sauti kubwa sana nyuma yake.

"Ni sawa," Tin alisema akicheka. "Nafikiri Noodle anataka kuwa mmoja wa bendi la We Can Band. Na nafikiri anataka kujiunga nasi pia," alisema akimnyoshea kidole Bella.

Tin alimsaidia Bella kupanda jukwaani na kusaidia kutoa mikebe ya kengele kutoka kwa mwili wa Noodle. Kisha Bella na Noodle walienda na kusimama karibu na Neo, Hope na Josh.

Tin alicheza gitaa yake na kusema, "HEBU TUCHEZE MUZIKI!"

Tin aliwanyoshea kidole Neo na Hope, walipiga ngoma zao. Kisha Tin akaimba, "Mguu wa kushoto nyuma," na kunyooshea kidole umati.

"Mguu wa kushoto nyuma," umati uliimba.

Kisha Tin akamnyoshea kidole Josh na akatikisa vitikisi vyake kuendana na mdundo wa muziki.

"Mguu wa kushoto kulia," Tin aliimba.

"Mguu wa kushoto kulia," umati uliimba.

Tin alimnyoshea kidole Bella. Mikebe iliyo kwenye laini ilitoa sauti nyororo wakati Bella aliigonganisha. Noodle alitoa sauti ya furaha.

Punde si punde tafrija ilipendeza sana. Tin aliimba nyimbo zake huku Neo, Hope, Josh na Bella wakicheza naye. Na Noodle aliimba kwa sauti kila mara ili kushiriki pia!

Kisha kila mmoja wa wasanii wengine waliimba nyimbo kutoka nchi zao. Umati ulishangilia na kupiga makofi. Walipendezwa na burudani hiyo!

"Mmeona," Tin alisema kwa bendi la We Can Band, "timu hii ndogo imetimiza ndoto! Asanteni kwenu nyinyi wanne ... naNoodle, kila mtu alifurahia tafrija hiyo!"



Familia ambazo husoma pamoja, hufaulu pamoja

Soma na uhadithie KILA mtoto KILA siku

Unaweza kusoma hadithi kwa sauti kwa watoto wenye umri wa miaka 6 na zaidi. Watoto wenye umri wa miaka 3 hadi 6 watafurahia *kusikiliza* hadithi unapowahadithia. Yafuatayo ni mawazo kuhusu jinsi ya kushiriki hadithi na watoto wenye umri mdogo.

Kabla

- ★ Elewa hadithi vizuri zaidi ili uweze kuihadithia kwa njia yako mwenyewe.
- ★ Fikiria jinsi ya kufanya hadithi iwe ya kuchangamsha.
 - Tayarisha bango linalosema: "Njoo kwenye karamu yetu katika bustani!" Bandika bango mahali ambapo watoto wataliona.
 - Chagua muda ambao familia yako iko pamoja.
 - Tafuta sehemu za hadithi ambapo watoto wanaweza kujiunga, kwa mfano, kufanya vitendo kulingana wimbo wa Tin.
 - Amua kuhusu sura na ishara ambazo ungependa kutumia unaposimulia hadithi, kwa mfano, kutafuta We Can Band kama vile Neo alivyofanya.
 - Kusanya na/au utengeneze ngoma, ala za kutikisa na kengele kwa kutumia mikebe, au upakue na uchapishe picha za hadithi kutoka kwenye tovuti ya www.nalibali.org ili uzitumie na kuzionyesha unaposimulia hadithi.
- ★ Fanya mazoezi ya kusimulia hadithi wewe mwenyewe au uruhusu kila mhusika kwenye hadithi isomwe na mhusika au rafiki tofauti. Kwa mfano, sehemu ya Gogo inaweza kusimuliwa na Gogo wenyu mwenyewe.

Wakati

- ★ Tambulisha hadithi na wahusika.
- ★ Wasimulie watoto hadithi.

Baada

- ★ Uliza maswali ya wazi ili kuwatia moyo watoto wafikirie na kuzungumza kuhusu dhana zinazohusiana na hadithi, kwa mfano, "Ni kitu gani unachopendelea kufanya ukiwa kwenye karamu?"
- ★ Kwa pamoja, chezeni densi ya kupiga hatua. Taja hatua mnazopiga jinsi Tin alivyofanya.
- ★ Alika watoto:
 - watengeneze ala za muziki kama vile ngoma, ala za kutikisa na kengele kutoka kwenye vitu vilivyotumika kama vile mikebe, plastiki, uzi au kamba, tishu, shanga, vifungo vya nguo na vifuniko vya chupa, pamoja na gundi, makasi na rangi.
 - buni maonyesho ya muziki ambapo watacheza ala zao na kuimba.
 - tengeneza matukio kutoka kwenye hadithi kwa kutumia udongo wa kauri au mfano wa udongo wa kauri wa watoto kuchezea.



Shiriki picha na video zinazokuonyesha wewe na watoto wako mkifurahia hadithi ya **Siku ya Kusoma kwa Sauti Duniani** na shughuli mnazofanya kwenye ukurasa wa Facebook!



Nal'ibali (ni neno la Kikosa linayomaanisha "hii hapa hadithi") ni kampeni ya kitaifa ya kusoma kwa ajili ya kufurahia. Dhamira yetu ni kuwa na nchi ya Afrika Kusini ambapo **kila mtoto anafurahia kusoma/kusikiliza hadithi kila siku.**

Kampeni ya Nal'ibali imebuniwa ili kukutia motisha na kukusaidia. **Wasiliana nasi** kwa njia yoyote kati ya hizi:

f nalibaliSA

t @nalibaliSA

@nalibaliSA

✉ info@nalibali.org

Nal'ibali

SWAHILI